

JUHA HAFUNDISHIKI

1. Hata ukifanya nini, juha hawafundishiki,
Kiwafanyia hisani, kitaka kuwabariki,
Kiwapeleka shuleni, yao hayaeleweki!
Juha hawafundishiki, hata ukifanya nini!
2. Jipumzishe nyumbani, sikhofu yao mikiki,
Ya Ustadh tulizani, sijali yao mikuki,
Kali haina aslani, si hatari ya bunduki!
Juha hawafundishiki, hata ukifanya nini!
3. Hawoni yako hisani, wao ni kukuhakiki,
Kukashifu hadharani, hawajui lilo haki,
Jitulize barazani, kula yako mishikaki!
Juha hawafundishiki, hata ukifanya nini!
4. Kalamu naweka chini, beti nne naafiki,
Jitulize Washingtoni, wala usitaharuki,
Ajitosae mtoni, kuzama atadiriki!
Juha hawafundishiki, hata ukifanya nini!

HAU
Cologne, Germany.